



*Taarifa kwa Vyombo vya Habari, 02 Mei 2015*

## **Serikali yachelewesha tena vitabu vya Bajeti kwa wabunge**

Serikali kwa mara nyingine imeshindwa kuwapatia wabunge vitabu vya makadirio ya bajeti siku 21 kabla ya kikao cha Bunge la bajeti kuanza. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 96 ya Kanuni za Kudumu za Bunge (toleo la 2007).

Pamoja na kuwepo kwa mwongozo huo, taarifa kutoka kwa wabunge kadhaa waliozungumza na Sikika kati ya tarehe 23 na 30 Aprili, 2015 inaonyesha kwamba nakala za vitabu vya bajeti havijawafikia wabunge. “Hatujapokea vitabu vya makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/16 wakati tunategemea kuanza kwa kikao cha bajeti. Pamoja na juhudi zetu za kufuatilia nyaraka hizi kama ilivyoelekezwa katika kanuni za Bunge lakini utekelezaji wa watendaji wa serikali umekuwa ni wa shida sana. Hii hutupa tabu katika kushiriki mijadala ya kuiboresha bajeti husika” alisema mmoja wa wabunge hao, Mh. Faki H. Makame (CUF - Mtoni-Zanzibar).

Sikika pia ilitembelea tovuti ya Bunge pamoja na ya Wizara ya Fedha na kubaini kwamba, hadi tarehe 30 April, takribani siku 5 tu kabla ya kuanza kwa kikao cha bajeti, wabunge walikuwa bado hawajapatiwa vitabu vya bajeti ambavyo ni nyaraka muhimu kwa utendaji wao. Kikao cha 20 cha Bunge la bajeti kinatarajiwa kuanza Mei 12, (2015)

Kwa takribani miaka mitano (5) sasa, Sikika imekuwa ikiikumbusha serikali kupitia Wizara ya Fedha pamoja na ofisi ya Bunge kutoa nakala za makadirio ya bajeti kwa wabunge na wananchi kulingana na kanuni. Vilevile imekuwa ikiwataka wabunge kudai nyaraka hizi muhimu kwa utendaji wao, lakini jitihada hazijaweza kuzaa matunda kwakuwa serikali haijawahi kuwapatia wabunge nyaraka hizo kwa wakati, bila sababu za msingi.


Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), Ibara 63 (3) na 137 zimeleza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka, kwa niaba ya wananchi "*kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote.*" Ili kutekeleza kiufanisi kazi yao ya kuidhinisha matumizi ya bajeti, wabunge wanahitaji muda wa kutosha wa kupitia nyaraka hizo na kujadili na wananchi wao,

ambao kimsingi ndio wenye mamlaka juu ya serikali. Lengo lingine ni kuona kama vipaumbele vya wananchi vimehusishwa au kama kuna marekibisho yoyote.

Hivyo basi, kutosambazwa kwa wakati vitabu vya makadirio ya bajeti kwa wabunge na umma kwa ujumla kunaathiri misingi ya kukuza uwazi, ubora na ufanisi katika bajeti. Lakini pia, kuchelewa kukabidhiwa kwa nyaraka hizi kwa wabunge kunaweza kusababisha uchambuzi duni kwa mipango ya fedha na pia kukosa maoni kutoka kwa wananchi wanaowawakilisha. Na zaidi, wanaweza kuwa katika hatari ya kupitisha makadirio ya bajeti yasiyokidhi mahitaji yenye kuakisi hali halisi ya wananchi.

Kucheleweshwa kupata vitabu pia kunawafanya wabunge wasipate muda wa kutosha wa kupitia na kubaini mapungufu kama yapo. Kwa ujumla, utendaji wa aina hii haulengi kuliletea taifa tija bali kulididimiza hasa kwa kuwa unakinzana na dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika kuandaa na kupitisha mipango ya mandeleo ya taifa letu.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawapa wabunge mamlaka ya kuwahoji mawaziri kuhusu mambo yenye maslahi kwa umma na kupatiwa ufafanuzi. Hivyo basi, tunatoa rai kwa Bunge letu tukufu kumwajibisha Waziri Mkuu ambaye ni kiongozi wa shughuli za serikali bungeni, anayepaswa kuhakikisha bajeti zinapatikana kwa wakati. Pia, tunawataka wabunge wahoji na kudai ufumbuzi wa tatizo hili ili vitabu visicheleweshwe tena katika vikao vya bajeti vijavyo.



Mr. Irenei Kiria, Mkurugenzi wa Sikika, S.L.P 12183 Dar es Salaam,

Simu: +255 222 666355/57, Nukushi: 2668015, Barua pepe: [info@sikika.or.tz](mailto:info@sikika.or.tz),

Twitter: [@sikika1](https://twitter.com/sikika1), Facebook: [Sikika Tanzania](https://www.facebook.com/SikikaTanzania), Tovuti: [www.sikika.or.tz](http://www.sikika.or.tz)